

**HOTUBA YA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU
HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA, KWENYE UZINDUZI WA MITAMBO
MIPYA YA MATATIBU YA MOYO KATIKA TAASISI
YA MOYO YA JAKAYA KIKWETE
DAR ES SALAAM, TAREHE 12 JUNI, 2021**

*Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, Waziri wa Afya,
Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;*

*Mheshimiwa Amos Makalla,
Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;*

*Ndugu Kate Kamba, Mwenyekiti wa CCM,
Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na
Viongozi wote wa Vyama vya Siasa;*

Waheshimiwa Viongozi wa Dini;

*Prof. Abel Makubi, Katibu Mkuu, Wizara ya Afya,
Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;*

Dkt. Aifello Sichwale, Mganga Mkuu wa Serikali;

*Prof. William Mahalu, Mwenyekiti wa Bodi ya
Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete;*

*Prof. Lawrence Maseru, Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali
ya Taifa ya Muhimbili;*

*Prof. Mohamed Janabi, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi
ya Moyo ya Jakaya Kikwete;*

Waheshimiwa Mabalazi mliopo;

Wafanyakazi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete;

Wageni Waalikwa, Wana-Habari, Mabibi na Mabwana;

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa
Tanzania!**

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi
Mungu, muumba wetu, kwa kutujalia uhai na kutuwezesha
kukutana leo hapa. Aidha, nakushukuru Mheshimiwa

Waziri wa Afya na Uongozi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete kwa kunialika kwenye tukio hili muhimu la uzinduzi wa Mitambo miwili ya kisasa ya Uchunguzi na Tiba ya Maradhi ya Moyo: *Catheterization Laboratory* (au Cath Lab) pamoja na Carton 3 kwa gharama ya **shilingi bilioni 4.6**. Ahsanteni sana.

Nawashukuru pia wageni wenzangu wote waalikwa kwa kuhudhuria hafla hii. Nimefurahi pia kuwaona waheshimiwa Mabalizi mbalimbali. Hii inaonesha kuwa mnatambua uzito na umuhimu wa tukio hili.

Waheshimiwa Viongozi,

Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;

Hivi punde tumesikia kuwa magonjwa yasiyoambukiza (moyo, figo, kisukari, saratani au kansa, n.k.) yanaongezeka duniani. Kwa mujibu wa Takwimu za

mwaka 2016, magonjwa haya yalisababisha zaidi ya vifo **milioni 41**, sawa na **asilimia 71** ya vifo vyote vilivyotokea. Takwimu pia zinaonesha kuwa, magonjwa ya moyo na shinikizo la damu ndiyo yenye kuongoza kwa kusababisha vifo. Kwa hapa nchini, takwimu zinaonesha kuwa magojwa yasiyoambukiza yalichangia **asilimia 33** ya vifo vyote nchini mwaka 2017, ambapo vifo vilivyotokana na magonjwa na moyo na shinikizo la damu vilikuwa **asilimia 13**.

Ni kwa kuzingatia hilo, leo tuna faraja kuweza kuzindua mitambo hii miwili ya kisasa ya uchunguzi na tiba ya magonjwa ya moyo. Kama tulivyosikia, Mtambo wa *Cath Lab* tulioununua ni wa kisasa ukilinganisha na mtambo uliokuwepo awali. Aidha, Mtambo wa *Carton 3* utatufanya tuwe miongoni mwa nchi 8 Barani Afrika yenye Mitambo ya namna hiyo. Kununuliwa kwa mitambo hii kutaimarisha

uwezo wetu wa kuchuguzwa na kutibu magonjwa ya moyo, ikiwemo kufanya upasuaji wa moyo, uchunguzi wa mishipa ya moyo, kuziba matundu ya moyo, pamoja na kurekebisha mapigo na mfumo wa umeme wa moyo.

Napenda kutumia fursa hii kuzishukuru Awamu ya Nne na ya Tano za Uongozi wa nchi yetu kwa jitihada walizofanya hadi tumefika hapa. Kama tulivyosikia, Hospitali hii ilianza wakati wa Awamu ya Nne; lakini imepata mafanikio makubwa wakati wa Awamu ya Tano. Hivyo basi, nazipongeza sana Awamu hizo za Uongozi wa nchi yetu. Kwa namna ya pekee sana, nawashukuru na kuwapongeza sana Uongozi, Madaktari pamoja na Wauguzi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete kwa kazi nzuri waliyofanya. Kama tulivyosikia, tangu taasisi imeanzishwa jumla ya wagojwa **5,959** wamepata huduma za upasuaji wa

moyo kwa kutumia tundu dogo, ambapo ni watu **11** tu ndiyo wamepoteza maisha baada ya upasuaji, sawa na **asilimia 0.2**. Mwandishi mkongwe wa Vitabu wa Marekani Bw. Elbert Hubbard aliwahi kusema *“One machine can do the work the work of fifty ordinary men; but no machine can do the work of one extraordinary man”*. Hii inaonesha kuwa pamoja na mitambo iliyopo, kazi kubwa inafanywa na madaktari. Mitambo haifanyi kazi yenyewe, bali inasimamiwa na kutumia na madaktari pamoja na wauguzi.

Kabla ya kuja hapa, nimetembelea maeneo mbalimbali ya Taasisi hii. Nimeelezwa na kushuhudia mambo makubwa, ikiwemo jinsi moyo unavyosimamishwa kabla ya kufanya upasuaji. Nimejionea pia picha za jinsi madaktari wanavyofanya kazi. Hivyo, narudia tena kuwapongeza madaktari na wauguzi wa Taasisi ya Jakaya Kikwete kwa

kazi nzuri mliyoifanya. Kutokana na kazi yenu nzuri, mmeweza pia kuokoa kiasi kikubwa cha fedha. Gharama za kutibu idadi ya wagonjwa niliyoitaja ni **shilingi bilioni 205.585** bila kujumlisha nauli; lakini kwa hapa nchini, matibabu yamegharimu **shilingi bilioni 104** na hivyo mmeokoa kiasi cha **shilingi bilioni 101**. Hongereni sana; na nataka niwaahidi kuwa, Serikali itaangalia maslahi yenu. Sambamba na hilo, tumesikia kuwa baadhi ya wagonjwa wanatibiwa kwa msamaha wa Serikali; hivyo, tumepokea ombi lenu ili angalau **asilimia 30** kwa kuanzia ilipwe kwenye Hospitali hii, ili kuendeleza huduma.

Waheshimiwa Viongozi, Mabibi na Mabwana;

Nimefarijika kusikia kwamba miongoni mwa waliotibiwa hapa ni wagonjwa kutoka Burundi, Comoro, Ethiopia, Malawi, Marekani, Misri, Rwanda, Uganda,

Ugiriki, n.k. Hii ni hatua nzuri kuelekea azma yetu ya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha utoaji huduma za kibingwa na ubingwa bobenzi Barani Afrika lakini pia kukuza utalii wa matibabu (*Medical Tourism*). Kwa mujibu wa utafiti wa *Patients Beyond Borders*, inakadiriwa kuwa, kila mwaka, takriban watu **milioni 14** hadi **milioni 16** husafiri kufuata huduma za matibabu sehemu mbalimbali duniani, ambapo inakadiriwa wanatumia kiasi cha **Dola za Marekani bilioni 45.5** hadi **bilioni 72**.

Napenda kutumia fursa hii kutoa shukran nyingi kwa nchi mbalimbali marafiki ambao wanashirikiana nasi katika kuimarisha huduma za moyo za kibingwa bobenzi, ikiwemo Australia, China, Falme za Kiarabu, India, Israel, Marekani, Misri na wengineo. Kama nilivyosema awali, nimefurahi

baadhi ya Mabalazi hao wako hapa. Naomba mpokee shukrani zetu na tunawasihi sana mzidi kushirikiana nasi.

Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;

Dhamira ya Serikali ni kuboresha na kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya nchini. Hivyo basi, mbali na ununuzi wa mitambo hii ya Taasisi ya Moyo, tumeimarisha pia huduma za afya kwa magonjwa mingine yasiyoambukiza, ikiwemo kisukari na saratani. Nakumbuka mwezi Machi 2019, wakati nikiwa Makamu wa Rais, nilizindua mashine ya kisasa ya tiba ya mionzi inayojulika kwa jia la *Linear Accelerator* (LINAC) iliyogharimu **shilingi bilioni 9.5** Aidha, Serikali imetoa **shilingi bilioni 14.5** kununua mtambo wa PET SCAN. Vilevile tumeimarisha huduma za matibabu ya figo katika Hospitali ya Taifa

Muhimbili na Benjamin Mkapa na pia kuanzisha huduma za ugonjwa wa Seli Mundu katika hospitali zote za mikoa.

Sambamba na hilo, Serikali hivi sasa inaendelea na ujenzi, upanuzi na ukarabati wa miradi **22** ya miundombinu ya hospitali za rufaa za mikoa, kanda na hospitali maalum, vikiwemo vyumba vya wagojwa wa dharura na mahututi, kwa gharama ya takriban **shilingi bilioni 193**. Aidha, kwenye bajeti ya mwaka huu, tumepanga kuendeleza ujenzi wa hospitali za wilaya **99** na kuanza ujenzi wa hospitali mpya za wilaya **28**; kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya **52** na kuanza ujenzi wa vituo vipya **121**; na pia kukamilisha ujenzi wa maboma ya zahanati **763**. Gharama za ujenzi wa miradi hii ni **shilingi bilioni 198.15**. Zaidi ya hapo, tumetenga **shilingi bilioni 263** kwa ajili ya kununua dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na kama alivyosema

Mheshimiwa Waziri wa Afya, tumetoa kibali cha ajira za watumishi wa afya wapatao 3,337. Ni matumaini yangu kuwa hatua hizi zitapanua wigo, zitaboresha na kuimarisha utoaji na upatikanaji wa huduma za afya nchini.

*Mheshimiwa Waziri wa Afya;
Waheshimiwa Viongozi mliopo;
Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;*

Kabla sijahitimisha hotuba yangu, napenda kutumia fursa hii, **kwanza**, kuihimiza Wizara, Madaktari, Wauguzi pamoja na watumishi wote wa afya kuhakikisha mnaitunza na kuwa na utaratibu wa kufanya ukarabati na matengenezo ya miundombinu na mitambo inayojengwa na kununuliwa na Serikali. Waswahili husema “*kitunze kidumu*”. Nimefurahi kuona ndani ya Taasisi hii kuna mafundi ambao wanakagua na kuifanyia marekebisho/matengenezo mitambo.

Pili, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi hii amewasilisha maombi matatu: maombi ya fedha za ujenzi wa jengo jipya la Taasisi hapa Muhimbili litakalogharimu takriban **bilioni 4**, ambapo ameiomba Serikali kutoa fedha za bajeti ya maendeleo iliyopitishwa ya **shilingi bilioni 2** na kuomba kiasi kingine kilichobaki. Na huu ndiyo mfano tunaotaka. Taasisi imefanya kazi na kupata kiasi cha fedha; na kuomba waongezewe kiasi kilichosalia. Nataka niwahakikishie kuwa Serikali itawapatia kiasi cha **shilingi bilioni 2** mlizoomba.

Maombi mengine ni kuhusu ujenzi wa ofisi mpya kule Mloganzila, ambapo ardhi imepatikana na Mkataba tayari umesainiwa na marafiki zetu wa China. Serikali itafuatilia suala hilo ili kuhakikisha kwamba Jengo linajengwa kama tulivyokubaliana na ndugu zetu wa China. Mwisho, ni

kuhusu kibali cha ajira kwa wataalam 12 ambao wanafanya kazi kwenye Taasisi hii, wakiwemo madaktari bingwa watatu. Tumeyapokea maombi hayo; na tutayafanyia kazi ili kuendeleza kazi nzuri ilianzishwa na Awamu zilizotangulia.

Mwisho kabisa, Prof. Mahalu amezungumzia umuhimu wa kuanzisha Vituo vya Taasisi hii kwenye kila Mkoa. Ni jambo zuri; lakini zaidi ya hapo, upo umuhimu pia wa kufanya utafiti wa magonjwa haya yasiyoambukiza.

Baada ya kusema hayo, na kwa kuwa, tayari nilishazindua mitambo ya *Cath Lab* na *Carto 3*.

Mungu Ibariki Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete!

Mungu Ibariki Tanzania!

*Nawasalimu tena kwa Jina la Jamhuri
ya Muungano wa Tanzania!*

“Asanteni Sana kwa kunisikiliza”